

Namba ya Mtahiniwa_____

Jina la Shule_____

Wilaya_____

Mkoa_____

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI MTIHANI WA UTAMILIFU WILAYA



DARASA LA SABA - MEI 2024 SOMO: KISWAHILI [01]

Muda: Saa 1:40

Tarehe:.....

MAELEKEZO

1. Mtihani huu una sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali Sita (6)
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu
3. Majibu yote yaandikwe katika karatasi hii
4. Tumia kalamu ya wino wa rangi ya bluu au mweusi
5. Simu za mikononi na vifaa vingine visivyohitajika haviruhusiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika kwa usahihi **Namba yako** na **Jina la Shule** kwenye sehemu ulizopewa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mtahini
1		
2		
3		
4		
5		
6		
Jumla		
SAHIHI YA MHAKIKI		

SEHEMU A:

1. Chagua herufi ya jibu sahihi na andika katika kisanduku.

- i. Kwa mujibu wa habari hii hayo mafunzo yalikuwa yanahusu nini?
(a) Elimu (b) Ushauri nasaha (c) Utandawazi
(d) Uhujumu uchumi (e) Unyanyasaji []
- ii. Kutokana na habari hiyo takwimu inaonyesha mwaka jana wanafunzi wangapi walipata mimba wakashindwa kuhudhuria masomo.
(a) 402 (b) 420 (c) 102
(d) 204 (e) 2001 []
- iii. Mafunzo hayo yaliongozwa na nani?
(a) Afisa elimu (b) Afisa afya (c) Afisa ustawi wa jamii
(d) Afisa kilimo (e) Afisa mipango miji []
- iv. Mwandishi anasema mafunzo hayo yaliendeshwa kwa muda wa siku ngapi?
(a) Tano (b) Tatu (c) Mbili
(d) Sita (e) Moja []
- v. Lengo kuu la mafunzo hayo lilikuwa ni _____
(a) Kujitambua (b) Kujithamini (c) Kujihimu
(d) Kujikwamua (e) Kujiimarisha []

2. Chagua herufi ya jibu sahihi.

- i. Sengambule si ndugu yangu. Neno "si" limetumika kama aina gani ya maneno?
(a) Kivumishi (b) Ukanushi (c) Kiwakilishi
(d) Kitenzi (e) Kihusishi []
- ii. Niliposomea uhandisi ndipo pazuri. Wakati ujao wa sentensi hii utakuwa _____
(a) Niliposomea uhandisi sio pazuri (b) Tutakaposomea uhandisi ndipo pazuri
(c) Tunaposomea uhandisi ndipo pazuri (d) Nitakaposomea uhandisi ndipo pazuri
(e) Nitakaposomea ni pazuri []
- iii. Saidi amempigia babu simu kumjuza msiba wa mwanaye. Mtendwa ni nani?
(a) Saidi (b) Babu (c) Simu
(d) Msiba (e) Mwanaye []
- iv. "Mwanagu anasoma shule nzuri". Kauli taarifa ya sentensi hii itakuwaje?
(a) Alisema mwanangu anasoma shule nzuri
(b) Alisema kuwa mwanangu anasoma shuleni
(c) Alisema kuwa mwanaye anasoma shule nzuri
(d) "Mwanaye anasoma shule nzuri"
(e) Mwanangu anasoma `shule nzuri []
- v. "Ninapenda kusoma kitabu kizuri". Nafsi ya tatu wingi wa sentensi hii ni?
(a) Tunapenda kusoma kitabu kizuri (b) Anapenda kusoma kitabu kizuri
(c) Unapenda kusoma kitabu kizuri (d) Wanapenda kusoma kitabu kizuri
(e) Ninapenda kusoma kitabu kizuri []
- vi. Ambao wamechaguliwa wapite mbele lakini wasikae kwenye madawati. Hii ni aina gani ya sentensi.
(a) Sahili (b) Shurutia (c) Kuu
(d) Changamano (e) Ambatano []

- vii. Changarawe ni mchanga madhubuti wa kujengea, kisawe cha neno madhubuti ni _____
 (a) Dhaifu (b) Nzuri (c) Imara
 (d) Mchafu (e) Mwepesi []
- viii. Huyu mtoto ni mwizi hapa mtaani ijapokuwa anatusaidia kulinda usiku. Methali inayomfaa ni _____
 (a) Ivumayo haidumu
 (b) Sikio la kufa halisikii dawa (c) Baniani mbaya kiatu chake dawa
 (d) Mtaka yote kwa pupa hukosa yote (e) Hakuna ziada mbovu []
- ix. Chambuso ameamuriwa kucheza ngoma za jadi hadharani. Mtenda ni nafsi ya ngapi?
 (a) Tatu wingi (b) Pili wingi (c) Kwanza umoja
 (d) Tatu umoja (e) Kwanza wingi []
- x. Sangiwa angelijua _____ neno linalokamilisha sentensi hii ni
 (a) Angekuja (b) Angakuja (c) Asingekuja
 (d) Asingakuja (e) Asingelikuja []

3. Oanisha kifungu A na B ili kupata maana sahihi.

SEHEMU A			SEHEMU B	
i.	Maisha ya utusiutusi []	A.	Arusi kubwa	
ii.	Arusi ya ndovu kumla mwanaye []	B.	Mpaka asubuhi	
iii.	Mpaka liamba []	C.	Kitu kinachotegemewa sana	
iv.	Uti wa mgongo []	D.	Ugomvi mkali	
v.	Ubavu kwa ubavu []	E.	Mifupa ya migongoni maisha yasiyokuwa na matumaini	
		F.	Mpaka usiku	
		G.	Sambamba	

SEHEMU B

4. Panga sentensi zifuatazo kwa kuzipa herufi A - E kwa mtiririko wenye maana.

- i. Ndipo kikaanzishwa chama kimoja cha mapinduzi (CCM). []
- ii. Kabla ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992. []
- iii. Usitishwaji wa mfumo wa vyama vingi ulifanyika mwaka 1965. []
- iv. Kilidumu kwa muda wa miaka 15. []
- v. Ambao uliimarisha demokrasia. []

5. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali ya kipengele (I - IV)

Kidato nimemaliza, tangu ule mwaka jana,
Maswali nimemaliza, kwa walimu na wajuzi,
Mingi pia nimecheza, michezo kwao ujuzi,
Sanaa nayo elimu, shuleni sijakutegea.

Najionea fahari, kuitwa mtaalamu
Napata nyingi fahari, kwa wangu utaalumu,
Sitachoka kukariri, nilopata kwa walimu,
Elimu kitu muhimu, usilaumu walimu.

Utakosa uhondo, neema tele na raha,
Kumbukizi la mikondo, sikuliona fedheha
Nyota pia na vimondo, havikunipa jeuri
Elimu nguzo muhimu, pata ukajionee.

MASWALI

- i. Shairi ulilosoma lina jumla ya beti zilizokamilika ngapi

- ii. Neno fedheha kama lilivyotumika katika ubeti wa tatu lina maana gani?

- iii. Shairi ulilosoma limetumia beti. Je, beti hizo zimetumia muundo gani?

- iv. Mkarara wa ubeti wa kwanza una vina na mizani. Andika vina vya mkarara huo

- v. Mshororo wa pili wa ubeti wa mwisho unakuwa na pande mbili, kipande cha pili cha mshororo huo kinaitwaje?

SEHEMU C

6. Tumia maneno kwenye kisanduku kukamilisha kadi ifuatayo

07144000, Dondodo,	wanayofuraha, S. S. Mtambo	13/3/2024,	Jumaa Yuzo,
-------------------------------------	---	-------------------	--------------------

Wananchi wa kijiji cha Rumba (i) _____ kukualika/kuwaalika ndugu, Dr, Mh.

(ii) _____ kwenye sherehe ya harusi ya mtoto wao,

itakayofanyika siku ya tarehe (iii) _____ katika ukumbi wa (iv) _____

uliopo mtakuja sokoni. Unaalikwa kuanzia saa 12:00 jioni - 3:00 usiku.

Tafadhali tumia mawasiliano haya kwa maelekezo zaidi (v) _____

Namba ya Mtahiniwa_____

Jina la Shule_____

Wilaya_____

Mkoa_____

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI MTIHANI WA UTAMILIFU WILAYA



DARASA LA SABA - MEI 2024

SOMO: URAIA NA MAADILI [06]

Muda: SAA 1:30

Tarehe:

MAELEKEZO

1. Mtihani huu una sehemu **A, B na C** zenye jumla ya maswali **Sita (6)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu
3. Majibu yote yaandikwe katika karatasi hii
4. Tumia kalamu ya wino wa rangi ya **bluu** au **mweusi**
5. Simu za mikononi na vifaa vingine visivyohitajika **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika kwa usahihi **Namba yako** na **Jina la Shule** kwenye sehemu ulizopewa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mtahini
1		
2		
3		
4		
5		
6		
Jumla		
SAHIHI YA MHAIKI		

SEHEMU A: (ALAMA 20)

Chagua jibu sahihi kwa kuandika herufi kwenye kisanduku.

1. i) Kutoa msaada ni muhimu sana katika jamii. Misaada hii huwa ya aina mbalimbali. Mtu kupewa msaada hutegemeana na nini? (a) Uhitaji kwa wakati huo
(b) Umaarufu wa mtaji (c) Kutegemeana na uwezo wa mtu
(d) Kutegemeana na mazingira ya mtu
(e) Kutegemeana na wingi wa wanaohitaji msaada []
- ii) Tabia ya kupenda kuwatendea wengine wema hata kama haulipwi na mtu huitwa?
(a) Uonevu (b) Utajiri (c) Wema
(d) Hisani (e) Uzuri []
- iii) Andiko la mwanzo kabisa la jambo fulani kabla ya kufanyiwa marekebisha na kukubaliwa kuwa rasmi huitwa?
(a) Andiko kuu (b) Uchapaji (c) Mfumo
(d) Rasimu (e) Kawaida []
- iv) Hali ya kuheshimu kanuni na taratibu zilizowekwa na mamlaka zinazohusika bila kulazimishwa huitwa?
(a) Uwajibikaji (b) Kutii sheria (c) Kuepuka mgogoro
(d) Hehima (e) Busara []
- v) Mwalimu wa somo la uraia alisema kwamba kitendo cha kuthamini utu katika jamii huitwa?
(a) Thamani (b) Thamini
(c) Heshima (d) Upole (e) Maadili []
- vi) Uhusiano wa damu ambao watu hutokea katika uzao mmoja kutoka kizazi hadi kizazi huitwa?
(a) Uhusiano (b) Nasaba (c) Ujirani
(d) Upendo (e) Urafiki []
- vii) Mwalimu alisema ili tuwe wazalendo wa kweli hatuna budi kuimba wimbo wa Taifa na tamaduni zetu. Maneno hayo yaliwatia shauku kupenda Taifa. Je maneno hayo huitwaje?
(a) Maono (b) Kichocheo (c) Ushauri
(d) Maelekezo (e) Nasaha []
- viii) Tabia nzuri na mwenendo wa kupendeza unaowafanya wengine wawe na mvuto wa heshima kwako huitwa?
(a) Hadhi (b) Kabila (c) Tabasamu
(d) Haiba (e) Sanaa []
- ix) Uhusiano wa kiutendaji katika jamii kati ya mwanaume na mwanamke huitwa?
(a) Jinsia (b) Urafiki (c) Utendaji
(d) Uhusiano (e) Mke na mme []
- x) Mwalimu alisema chombo chenye mamlaka ya kuendesha utawala au siasa ya Taifa au nchi huitwa?
(a) Taifa (b) Mahakama (c) Katiba
(d) Dola (e) Kanuni []

2. Oanisha sehemu A na sehemu B ili kuleta maana

sehemu A	Jibu	Sehemu B
i) Ibara	[]	A. Sehemu au tawi la kampuni au taasisi fulani
ii) Ufundi	[]	B. Tendo la kufanya ubadhirifu au wizi wa mali zilizo katika dhamana yako
iii) Jinai	[]	C. Kifungu cha maneno yenye habari inayojieleza kimaana
iv) Tanzu	[]	D. Shitaka la uhalifu linalomsababishia mtu mashitaka
v) Mahakama	[]	E. Hutafsiri sheria na kutoa haki kwa wote

3. Jaza nafasi zilizoachwa wazi

**wima kwa ukakamavu, kulala, twiga, maziwa
1994, 1996, bahari, moto, mali simba**


- Mambo yote ya thamani ambayo mtu hujionea fahari kuwa nayo huitwa?

- Bendera ya Taifa inaitambulisha nchi ya Tanzania katika mataifa mengine bainisha rangi ya bluu katika bendera ya Taifa huwakilisha nini _____
- Moja ya tukio la kuhuzunisha ni lile la kuzama kwa MV Bukoba ambalo lilitokea mwaka gani? _____
- Unapoimba au kusikia wimbo wa Taifa unatakiwa kusimama katika hali gani?

- Miongoni mwa wanyama yupo ambaye anawakilisha nchi yetu ya Tanzania. Mnyama huyo anaitwa _____

SEHEMU B: (ALAMA 20)

4. Chunguza mchoro ufuatao kisha jibu maswali kwa makini.



- Chombo cha kutafsiri sheria zilizotungwa na Bunge na kutoa haki kwa wananchi wote huitwa?

- ii) Herufi A inawakilisha? _____
- iii) Herufi B inawakilisha? _____
- iv) Herufi C inawakilisha? _____
- v) Herufi D inawakilisha? _____

5. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika jibu sahihi.

- i) Hali ya mtu mmoja au kikundi cha watu kujikusanyia madaraka ya juu ya utawala
- ii) Sheria ya ndoa inayoruhusu mvulana akifikisha umri wa miaka 18 aoe ilikuwa ni sheria ya mwaka upi
- iii) Vitu muhimu vya thamani vinavyomilikiwa na nchi au Taifa huitwa
- iv) Mfumo wa maisha ya watu na jinsi wanavyoishi na taratibu zao kijamii, kiuchumi na kisiasa huitwa
- v) Kazi inayofanywa kwa makubaliano maalumu ya mkataba kama ujenzi wa barabara huitwa?

SEHEMU C: (ALAMA 10)

6. Chunguza mchoro ufuatao kisha jibu maswali yanayofuata.



- i) Eneo wanaloishi wanyama pori huitwaje? _____
- Taja maeneo hayo mawili unayoyajua yanayopatikana Tanzania
- ii) _____ iii) _____
- iv) Wanyama wanaopatikana eneo hilo huwa ni vivutio vya nini?

- v) Taja faida inayopatikana kwa Taifa kutokana na maeneo hayo

Namba ya Mtahiniwa _____
Jina la Shule _____
Wilaya _____
Mkoa _____

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI MTIHANI WA UTAMILIFU WILAYA



DARASA LA SABA - MEI 2024

SOMO: MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI [03]

Muda: SAA 1:30

Tarehe:

MAELEKEZO

1. Mtihani huu una sehemu **A, B na C** zenye jumla ya maswali **Saba (7)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu
3. Majibu yote yaandikwe katika karatasi hii
4. Tumia kalamu ya wino wa rangi ya **bluu** au **mweusi**
5. Simu za mikononi na vifaa vingine visivyohitajika **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika kwa usahihi **Namba yako** na **Jina la Shule** kwenye sehemu ulizopewa.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mtahini
1		
2		
3		
4		
5		
6		
7		
Jumla		
SAHIHI YA MHAIKI		

SEHEMU A: (ALAMA 20)

1. Chagua herufi ya jibu sahihi na andika katika kisanduku.

- i. Jumla ya mali alizonazo mtu au Taifa kwa ajili ya kujiendeleza kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni hujulikana kama _____
(a) Mali (b) Malighafi (c) Mchanga
(d) Rasilimali (e) Ubunifu []
- ii. Tanzania ni nchi iliyobarikiwa na mimea ya kutosha inayoota bila kupandwa katika eneo fulani. Bainisha mimea hiyo huitwaje?
(a) Mimea ya miti (b) Uoto wa asili (c) Uoto usio wa asili
(d) Uoto wa dhahabu (e) Uoto wa mbegu []
- iii. Uwindaji wa wanyamapori bila idhini kwa lengo la kupata mazao ya wanyamapori kama vile, pembe za ndovu, nyama na ngozi huitwa _____
(a) Ujambazi (b) Uwindaji (c) Ujangili
(d) Uharamia (e) Ubabaishaji []
- iv. Uhusiano wa viumbe na mazingira yao pamoja na viumbe wengine kitaalamu huitwaje?
(a) Undugu (b) Ujamaa (c) Mazingira halisi
(d) Ikolojia (e) Kemikali []
- v. Mwalimu wa somo la Maarifa alisema kuwa udongo unachembechembe ambazo ukizichunguza utagundua zimefanana. Hali hiyo huitwaje? _____
(a) Udongo mkali (b) Unamu (c) Usahili
(d) Urutubishaji (e) Changarawe []
- vi. Eneo la ardhi lenye kujaa maji kwa muda mrefu ukijumuisha mabwawa na delta ikiambatana na mimea inayostawi majini huitwa _____
(a) Ardhi anga (b) Ardhi maji (c) Kihoro
(d) Mabwawa makubwa (e) Ardhi oevu []
- vii. Rasilimali endelevu ambayo ikitumiwa huendelea kuwepo kwa mfano jua, hewa na upepo huitwa _____
(a) Rasilimali kuu (b) Rasilimali Umma
(c) Rasilimali jadidifu (d) Rasilimali kokoro
(e) Malighafi endelevu []
- viii. Rasilimali za kutengenezwa kama vile barabara, madaraja ya reli na bandari hujulikana kama _____
(a) Mali za Umma (b) Ujasiriamali
(c) Mbinu mbadala (d) Miundombinu
(e) Rasilimali endelevu []
- ix. Katika kijiji chetu cha Mkuranga kuna shamba maalumu linalotumika kufuga na kuzalisha mifugo. Je, aina ya mashamba hayo huitwaje?
(a) Shamba maalumu (b) Shamba la wanyama (c) Ranchi
(d) Shamba la watalii (e) Bungo []
- x. Wavu wenye matundu makubwa unaotegwa katika maji yenye kina cha wastani kwa ajili ya kuvua samaki huitwa _____
(a) Wavu mkuu (b) Jerife (c) Kokoro
(d) Nyavunyavu (e) Matundu []

- xi. Mafuta ya kupikia yanatokana na maziwa ya wanyama kama vile mbuzi huitwa _____
 (a) Samli (b) Jibini (c) Losheni
 (d) Mafuta mazito (e) Mafuta ya kula []
- xii. Uwekezaji wa mtaji katika biashara kwa lengo la kujijari na kujipatia kipato huitwa _____
 (a) Biashara (b) Wizi (c) Ujasiriamali
 (d) Uuzaji (e) Utangazaji []
- xiii. Ukitumia malighafi ya mbao kutengeneza viti, meza, kabati bidhaa hizi huitwaje kwa jina moja?
 (a) Thamani (b) Samani
 (c) Meza (d) Malighafi (e) Ufundi []
- xiv. Ukichunguza kuna misimu tofauti tofauti ya hali ya hewa. Bainisha msimu ambao ni wajua na usio wa mvua.
 (a) Vuli (b) Masika
 (c) Kiangazi (d) Kipupwe (e) Jua kali []
- xv. Mfululizo wa shughuli unaosababisha kitu fulani kufanyika au lengo kufikiwa huitwa _____
 (a) Fursa (b) Maono (c) Mchakato
 (d) Shughuli (e) Mtaji []

2. Oanisha Kifungu A na B ili kupata maana sahihi.

SEHEMU A			SEHEMU B	
i.	1961	[]	A.	Ajali ya garimoshi Dodoma
ii.	1967	[]	B.	Ajali ya maji MV. Bukoba
iii.	1996	[]	C.	Kifo cha Dkt. John Pombe Magufuli
iv.	2002	[]	D.	Tanganyika ilipata uhuru
v.	2021	[]	E.	Azimio la Arusha

SEHEMU B: (ALAMA 20)
Jibu maswali yote katika sehemu hii


3. a) Moja ya shughuli zinazofanywa na jamii zilizomo Tanzania ni ufugaji wa wanyama mbalimbali. Bainisha faida mbili zinazotokana na shughuli hiyo?
 i. _____
 ii. _____
- b) Zao linalopatikana Lindi, Mtwara na Pwani ni maarufu sana nchini Tanzania. Bainisha jina la zao hilo?

- c) Shughuli ya usafirishaji ni muhimu sana nchini. Eleza kwa ufupi umuhimu wa shughuli hiyo?

4. a) Bainisha njia mbili ambazo huweza kutumika kupunguza athari zinazotokana na upepo unaovuma kwa kasi.
 i) _____
 ii) _____
- b) Rasilimali ardhi ni moja ya msingi wa maendeleo ya kiuchumi katika taifa letu bainisha njia mbili za utunzaji wa rasilimali ardhi.
 i) _____
 ii) _____
- c) Ainisha shughuli mbili zinazochangia uharibifu wa rasilimali maji
 i) _____
 ii) _____
5. i. Jumla ya malighafi zinazokusanywa kutengeneza vitu mbalimbali huitwa _____
- ii. Mavazi ya aina mbalimbali ambayo muigizaji huyavaa wakati wa kuigiza kama sketi au kanzu _____
6. i. Ute mzito wenye rangi ya njano unaotanda juu ya maziwa huitwa _____
- ii. Chakula kitamu kinacholiwa baada ya mlo mkuu huitwaje _____

SEHEMU C: (ALAMA 10)

7. Chunguza mchoro ufuatao kisha jibu maswali.



MASWALI

- i. Herufi X huwakilisha

- ii. Herufi Y huwakilisha

- iii. Dunia hukamilisha mizunguko kulizunguka jua kwa muda wa siku ngapi?

- iv. Taja matokeo ya dunia kulizunguka jua

- v. Njia ambayo sayari ya dunia hupita kuzunguka jua huitwa

Namba ya Mtahiniwa _____

Jina la Shule _____

Wilaya _____

Mkoa _____

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI MTIHANI WA UTAMILIFU WILAYA



DARASA LA SABA - MEI 2024

SOMO: HISABATI [04]

Muda : Masaa 2

Tarehe:






MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali nane (8).
2. Jibu maswali yote.
3. Onesha wazi njia zilizotumika kujibu maswali yote katika nafasi iliyotolewa kwenye karatasi ya maswali.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi, isipokuwa katika michoro ambapo ni lazima kutumia penseli.
5. Vifaa vya mawasiliano visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika Namba yako ya Mtihani na taarifa nyingine zote muhimu katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mtaini
1		
2		
3		
4		
5		
6		
7		
8		
Jumla		
SAHIHI YA MHAKIKI		

NA	SWALI	KAZI NA JIBU
1.	<p>SEHEMU A: (Alama 10) Jibu maswali yafuatayo (Alama 10)</p> <p>i. $4,936,021 + 70,800 =$</p> <p>ii. $6,897,237 - 2,678,760 =$</p> <p>iii. $728 \times 35 =$</p> <p>iv. $12\frac{1}{4} \div 3\frac{1}{2} =$</p> <p>v. $160,000 \div 50 =$</p> <p>vi. $60.075 - 35.668 =$</p> <p>vii. $8\frac{1}{4} \div 4\frac{1}{2} =$</p> <p>viii. $9\frac{1}{4} - 3\frac{1}{2} =$</p> <p>ix. $(-7) + (-9)$</p> <p>x. $0.791 + 21.097 =$</p> <p>SEHEMU B: (Alama 30) 2 Jibu maswali yafuatayo:(Alama 6)</p> <p>i. Ilipofika saa 0045 Jafta alipiga kengele kwa nguvu. Unafikiri huo muda unaandikaje kwa muda huu kwa mfumo wa masaa 12;</p> <p>ii. Ukiambiwa ugawe miaka 18 na wiki 39 kwa saa 5</p> <p>iii. Shule ya msingi Bombambili ilijengwa mwaka 1936. Ikiwa Hamza alikuwa na miaka mitatu baada ya ujenzi huo. Je, mwaka 2024 Hamza ana umri gani? (Andika umri huo kwa namba za kirumi)</p>	

NA	SWALI	KAZI NA JIBU
iv.	Kipande cha kamba kina urefu wa sm 8.32 na upana wa sm 4.5. Tafuta eneo lake	
v.	Ngojera aliambiwa na mwalimu wake wa hisabati atafute zao la 789 na 56. Unafikiri alipata jibu gani?	
vi.	Ukiwambiwa kugawanya 10.96 kwa 0.008 Je, utapata jibu lipi?	
	3. Kokotoa maswali yafuatayo: (Alama 6)	
i.	Alice aliambiwa na mwalimu wake kutafuta namba mraba ya 9.89. Unafikiri alipata jibu gani?	
ii.	Kuna jumla namba shufwa ngapi kati 110 na 120.	
iii.	Zidisha $4\frac{2}{5}$ kwa $7\frac{1}{2}$ unafikiri jibu ni;	
	4 Jibu Maswali yafuatayo:(Alama 6)	
i.	Ukiwa mtaalamu wa hisabati; Badili 13.4% kuwa desimali	
ii.	Tafuta kigawe kikubwa cha shirika (KKS) cha 21, 24 na 28	
iii.	Tafuta kigawe kidogo cha shirika cha 12, 24 na 36	
	5. Kokotoa maswali yafuatayo (Alama 6)	
i.	Ikiwa 14:25 ni sawa na A:B ikiwa A= 70 Nini thamani ya B	
ii.	Gari lilisafiri umbali wa kilometer 120 kwa saa 1 na dakika 30. Tafuta speed ya gari hilo;	
iii.	Mpira alikuwa na mananasi 45 alimpatia Jane $\frac{4}{5}$ ya mananasi hayo. Je, alibakiwa na mananasi mangapi	

NA	SWALI	KAZI NA JIBU
6	<p>Jibu maswali yafuatayo (Alama 6)</p> <p>i. Idadi ya wanafunzi wa shule ya msingi Kizanda ni 480. Ikiwa wanafunzi 320 ni wavulana. Tafuta sehemu ya wanafunzi ambao ni wasichana.</p> <p>ii. Fumbua mlinganyo ufuatao; $6X - (X+2) = -3$</p> <p>iii. Jaza kigawe kinachokosekana katika ngoe hii thamani ya B</p> 	
7	<p>SEHEMU C: (Alama 10)</p> <p>i. Songambe huwa anapokea mshahara Songambe hutumia shilingi ngapi kwenye nyumba?</p>  <p>Tafuta gharama anazotumia Songambe kwenye chakula</p> <p>ii) Songambe hutumia sh. ngapi kwenye nyumba?</p> <p>iii. Tamari aliambiwa kuzunguka umbo lifuatalo. Je, unafikiri alilembea sentimeta ngapi?</p> 	
8	<p>i. Mwanafunzi aligawanya pembe mraba A, B, C na kupata pembe tatu kama inavyoonekana. Tafuta thamani ya y</p>  <p>ii. Ukiwa kama mtaalamu wa hisabati. Taja jina la umbo lifuatalo;</p> 	

Candidate's Number _____

School's Name _____

Region _____

District _____

BABATI DISTRICT COUNCIL

MOCK EXAMINATION ASSESSMENT



STANDARD SEVEN - MAY 2024

SUBJECT: ENGLISH [02]

Time: 1 Hour 40 Minutes

Date:

INSTRUCTIONS

1. This paper consists of sections A, B and C with a total of seven (7) questions.
2. Answer all questions in the spaces provided in this paper.
3. Section A and B carry twenty (20) marks each and section C carries ten (10) marks.
4. All writings must be in blue or black pen, except drawings which must be in pencil.
5. Communication devices and any unauthorised materials are not allowed in the examination room.
6. Write your Examination Number and all other important information at the top right corner of every page.

FOR EXAMINERS' USE ONLY		
Question Number	Score	Examiner's Initials
1		
2		
3		
4		
5		
6		
7		
8		
Total		
CHECKER'S INITIALS		

SECTION A: (20 MARKS)

1. Listen to the passage read by invigilator and then answer questions 1-5. (5 MARKS)

- i. What is the name of the leader led Tanzania according to the story?
(a) Dr. Samia Suluhu (b) J. K. Nyerere (c) Benjamin Mkapa
(d) John P. Magufuli (e) J. M Kikwete []
- ii. How many years left after the death of the leader
(a) 10 years (b) 12 years (c) 11 years
(d) 23 years (e) 20 years []
- iii. When the leader in the story born
(a) April 2002 (b) October 1999 (c) April 1922
(d) April 1942 (e) March 1922 []
- iv. The leader governed Tanganyika as prime minister from 1961 to _____
(a) 1999 (b) 2002 (c) 1922
(d) 1985 (e) 1962 []
- v. How long time did the leader led Tanzania as a president?
(a) ten years (b) twenty years (c) eleven years
(d) twenty one years (e) fifty years []

2. Choose correct answer (5 MARKS)

- i. The dog _____ running toward me
(a) are (b) they (c) we
(d) is (e) it []
- ii. _____Tanganyika and Eyasi are rift valley lakes
(a) both (b) not only (c) among
(d) then (e) but []
- iii. The doctor has told you what your problem is_____
(a) has he (b) hasn't you (c) has you
(d) hasn' t he (e) hasn't they []
- iv. We shall be late for school _____ we ran fast
(a) if (b) unless (c) because
(d) but (e) although []
- v. _____ you study hard, you will pass your examination
(a) unless (b) although (c) not only
(d) if (e) we []

3. Complete the given sentences (i - v) by writing the correct answer which given in the box (5 MARKS)

Why, When, Who, Which, Whose, Where

- i. _____ you came late everyday.
- ii. She told him _____ to put the suitcase.
- iii. This is the book _____ title I couldn't remember.
- iv. This is the desk in _____ I keep my books.
- v. Saturday is the day _____ I get my book.

4. Match items in List "A" with those in List "B" correctly (5 MARKS)

List "A"		List "B"
i. The boy is very weak []	A.	Our opponents gave up
ii. We played skilfully []	B.	I did not have to ask for help
iii. This animal is very dangerous []	C.	He was picked for the national team
iv. The question was very easy []	D.	He can not survive
v. He played well []	E.	It must be kept in a cage

SECTION B:

5. Fill in the blanks with the correct answer (10 MARKS)

- i. This is a girl _____ pen stolen yesterday
- ii. The money belongs to us. It is _____
- iii. This is your cow. It is _____
- iv. Use "either -----or " to fullfill the sentence
 _____ Jamila _____ Makonda is a fast learner
- v. Amina is too short _____ touch the roof

SECTION C: (20 MARKS)

6. Re-arrange the following sentences to get a meaningful passage by giving them letter (A-E) (10 MARKS)

- i. Then, we played a football match []
- ii. Although the football match was difficult, we won it []
- iii. On saturday morning, we started the journey to Songa Primary school []
- iv. When we arrived there, we started with the academic competition, but we lost it []
- v. Last wednesday, Our teacher told us that on saturday would go to Songa primary school for an-inter-school competition []

7. Read the poem below and answer the questions that follow (10 MARKS)

Listen, my child, there are no free things
If you want anything, work for it
Your labour is your pay
As they say, "No pain, no gain"

Not everything you see is someone's wish
It is normally the result of someone's labour, physical or mental
Being poor or rich usually is your choice
Your choice will make poverty continue or end

My beloved son, It's time for you to act
It is usually not late at your age
Beacause age determine your labour
Be a slave today in order to be a king tomorrow

Questions

- i. What is the poem about?

- ii. Who is speaking in the poem?

- iii. What message do you learn from the poem?

- iv. How many stanzas in the poem?

- v. What does "Be a slave today in order to be a king tomorrow" mean?

Namba ya Mtahiniwa _____

Jina la Shule _____

Wilaya _____

Mkoa _____

HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI MTIHANI WA UTAMILIFU WILAYA



DARASA LA SABA - MEI 2024 SOMO: SAYANSI NA TEKINOLOJIA [05]

Muda: Saa 1:30

Tarehe:

MAELEKEZO


1. Karatasi hii ina sehemu A B na C zenye jumla ya maswali nane (08).
2. Jibu maswali yote kwenye nafasi ulizopewa.
3. Sehemu A na B zina alama ishirini (20) kila moja na sehemu C ina alama kumi (10).
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi, isipokuwa katika michoro ambapo ni lazima kutumi penseli.
5. Vifaa vya mawasiliano na visivyo ruhusywa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika Namba yako ya Mtihani na taarifa nyingine zote muhimu katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU		
Namba ya Swali	Alama	Saini ya Mtaini
1		
2		
3		
4		
5		
6		
7		
8		
Jumla		
SAHIHI YA MHAIKI		


SEHEMU A: (ALAMA 20)

1. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi kwenye kisanduku kuanzia swali la i - x.


- i) Gesi ya oksijeni ni muhimu sana kwa wanyama katika upumuaji, gesi hii huweza kuzalishwa katika maabara kwa kutumia kompaundi mbali mbali chunguza mchoro ufuatao kisha bainisha herufi X.



- (a) umbijani (b) mwanga wa jua (c) hewa (d) joto (e) oksidi []
- ii) Wanyama wasio na uti wa mgongo wamegawanyika katika makundi makuu matatu. Bainisha kundi la wanyama wenye uti wa mgongo kati ya wafuatao?
- (a) tandu na jongoo (b) minyoo na nyungunyungu (c) konokono na minyoo
(d) ngisi na tandu (e) binadamu []
- iii) Gesi bwete ambayo hutumika kwenye taa za umeme na neli ang'avu za taa za umeme vilevile hutumika katika kukata na kuchomelea vyuma vya usafiri kama magari. Gesi hiyo huunda asilimia ngapi za hewa?
- (a) 78 (b) 20.9 (c) 0.03 (d) 0.9 (e) 0.17 []
- iv) Gesi inayotumika kwenye viwanda kwa ajili ya kusindika vinywaji vya aina mbalimbali kama vile soda na juisi huitwa _____
- (a) naitrojini (b) oksijeni (c) kabonidayoksaidi (d) agoni (e) heliam []
- v) Chunguza mchoro kuonesha aina moja wapo ya lenzi kisha bainisha sifa ya lenzi hiyo kati ya zifuatazo;



- (a) hukusanya miale ya mwanga
(b) hutawanya miale ya mwanga
(c) hurefusha miale ya mwanga
(d) husimamisha miale ya mwanga
(e) huwa haiakisi miale ya mwanga []
- vi) Miale mtuo ya mwanga hukutana katika nukta fulani baada ya kuakisiwa bainisha jina la nukta hivyo? (a) nukta nundu (b) folipo
(c) kiolwa (d) fokasi (e) bapa nundu []
- vii) Mwalimu wa Sayansi alifanya jaribio kuonesha tabia za usumaku hivyo alipanga sumaku katika ncha zinazofanana kama inavyoonekana. Bainisha nini kilitokea katika jaribio hilo?



- (a) ncha mbili zinazofanana huvutana (b) ncha mbili zinazofanana hukwepana
(c) ncha mbili zisizofanana hukwepana (d) ncha mbili zinazofanana husukumana
(e) ncha za sumaku zina kani inayolingana []

- viii) Nishati ya umeme huweza kuzalishwa kwa kutumia mawimbi ya maji bainisha mtambo wa kuzalisha umeme huwekwa sehemu ipi katika mkondo wa maji?
 (a) sehemu yenye kina kirefu (b) sehemu karibia na maporomoko
 (c) sehemu yenye mawimbi makubwa (d) sehemu karibu na kati ya maji
 (e) sehemu ambako chemchem ya maji huanza []
- ix) Dawa mbalimbali za kuulia wadudu na kuogeshea mifugo kuna mchoro ufuatao. Bainisha ni athari ipi unaweza kuipata endapo utashika vitu vyenye alama hii au kuingilia mwilini;



- (a) kuungua moto (b) kifo (c) ajali
 (d) kulipuka (e) kupata upofu []

- x) Mkondo wa umeme hupimwa na kipimo cha msingi cha kimataifa yaani kizio cha mkondo wa umeme ambacho huitwa _____
 (a) amita (b) kani (c) voltimeta (d) ampia (e) ometa []

2. OANISHA SEHEMU A NA SEHEMU B ILI KULETA MAANA.

SEHEMU A			SEHEMU B	
i)	Molekyuli	[]	A.	Kiasi au kipimo kilichokubalika kutumika kama vile ujazo (lita)
ii)	Atomu	[]	B.	Atomu zilizoungana pamoja na hushiriki katika pambano la kikemikali
iii)	Nyukliasi	[]	C.	Nguvu inayotokana na mvutano au msukumo wa molekyuli kwa ajili ya kuunganisha au kutenganisha vitu hivyo
iv)	Kizio	[]	D.	Chembechembe ndogondogo zinazounda molekyuli za maada na ambazo hazigawanyiki kwa urahisi
v)	Kani	[]	E.	Kiini cha katikati ya atomi

3. Jaza nafasi zilizowazi kwa usahihi.

Kikoa, seli, tahajia, mtandao janibu, kitabukazi, mtandao mpana sarufi

- i) Kisanduku cha mstatili ambacho hutokea kutokana na makutano ya safuwima na safumlalo kwenye mkeka kazi huitwa _____
- ii) Faili lenye mkusanyiko wa mkekakazi mmoja au zaidi huitwa _____
- iii) Mtandao ambao huunganisha tarakilishi ndani ya eneo dogo la kijiografia kwa mfano jengo la ofisi ya shule huitwa _____


- iv) Utambulisho unaofafanua mamlaka au udhibiti ndani ya intanenti
- v) Uwakilishaji wa sauti kwa herufi kufuatana na mwendelezo wa maneno uliokubalika

SEHEMU B: (ALAMA 20)
Jibu maswali yote katika sehemu hii

- 4. i) Kipanga aliloweka sare zake za shule na baadae alizifua na kuanika juani. Ainisha njia ya joto iliyosafiri kupitia hewa mpaka katika sare za kipanga
- ii) Kuta za themosi zilizopo katika chupa ya chai husaidia kuzuia joto kupungua. Bainisha kuta hizo zimetengenezwa kwa kutumia nini?
- iii) Sehemu ambayo ni tupu, isiyo na gesi wala hewa hujulikana kama
- 5. i) Osmosisi ni muhimu kwa seli na ogani za mwili wa kiumbe hai. Eleza kwa ufupi kwa nini ni muhimu?
- ii) Fafanua jina la kitendo ambacho husaidia wanyama kutambua walipo wanyama wengine
- iii) Eleza kwa ufupi kwa nini Osmosisi ni muhimu katika mimea?
- 6. i) Protini zilizopo kwenye plazima husaidia kuzuia kuvuja kwa damu kwenye mishipa. Fafanua kazi nyingine ya protini hizo
- ii) Seli nyeupe za damu hazina umbo maalumu hupatikana kwa uwingi katika damu. Eleza kazi kubwa inayofanywa na seli hiyo
- iii) Ainisha jina la ugonjwa unaosababishwa na virusi ambapo mtu hutokwa damu nyingi mwilini na kupasuka mishipa
- iv) Eleza kwa ufupi kwa nini mtu huweza kupata tatizo la kisukari

SEHEMU C: (ALAMA 10)
Jibu maswali yote katika sehemu hii.

7. Chunguza mchoro ufuatao ambao unaonesha gameti ume zinaenda katika gameti uke.



- i) Eleza mchoro huo unaonesha tendo gani?
- ii) Herufi Y imewakilisha
- iii) Herufi X imewakilisha
- 8. Iwapo jitihada ya kilogramu 24 ilitumika kunyanyua mzigo wa kg 72. Kwa umbali wa mita 6.
 - i) Tafuta manufaa ya kimakanika katika roda hiyo.
 - ii) Tafuta ufanisi wa roda hiyo iwapo jitihada ilijongea umbali wa mita 24.

HABARI YA KISWAHILI DRS VII - BABATI

Wanafunzi wa Shule ya Msingi za serikali wilayani Nachingwea wamehudhuria mafunzo ya ushauri nasaha. Mafunzo hayo yamefadhiliwa na jumuiya ya wazazi wa Wilaya hiyo. Yamefanyika katika ukumbi wa kilima juu, yaliongozwa na Afisa usatwi wa jamii, walimu na Afisa elimu wa wilaya hiyo. Mafunzo hayo waliendeshwa kwa muda wa siku tatu. Lengo kuu lilikuwa ni kujitambua kwa mujibu wa Afisa elimu. Walihudhuria wanafunzi 420 wa wilaya nzima. Viongozi wa wilaya waligutuka baada ya kugundua kuwa kila mwaka wanafunzi wengi huishia njiani bila kukamilisha masomo yao. Mfano mwaka jana wanafunzi 102 walipata ujauzito wakiwa shuleni hali iliyopelekea kushindwa kumaliza masomo.

HABARI YA KISWAHILI DRS VII - BABATI

Wanafunzi wa Shule ya Msingi za serikali wilayani Nachingwea wamehudhuria mafunzo ya ushauri nasaha. Mafunzo hayo yamefadhiliwa na jumuiya ya wazazi wa Wilaya hiyo. Yamefanyika katika ukumbi wa kilima juu, yaliongozwa na Afisa usatwi wa jamii, walimu na Afisa elimu wa wilaya hiyo. Mafunzo hayo waliendeshwa kwa muda wa siku tatu. Lengo kuu lilikuwa ni kujitambua kwa mujibu wa Afisa elimu. Walihudhuria wanafunzi 420 wa wilaya nzima. Viongozi wa wilaya waligutuka baada ya kugundua kuwa kila mwaka wanafunzi wengi huishia njiani bila kukamilisha masomo yao. Mfano mwaka jana wanafunzi 102 walipata ujauzito wakiwa shuleni hali iliyopelekea kushindwa kumaliza masomo.

ENGLISH PASSAGE - BABATI

Listen carefully the following passage and then answer the question 1 - 5.

He governed Tanganyika as prime minister from 1961 to 1962 and then as president from 1964 to 1985, He was born in April 1922 and passed away in october 1999. Then he led Tanzania as the president from 1964 to 1985

ENGLISH PASSAGE - BABATI

Listen carefully the following passage and then answer the question 1 - 5.

He governed Tanganyika as prime minister from 1961 to 1962 and then as president from 1964 to 1985, He was born in April 1922 and passed away in october 1999. Then he led Tanzania as the president from 1964 to 1985

ENGLISH PASSAGE - BABATI

Listen carefully the following passage and then answer the question 1 - 5.

He governed Tanganyika as prime minister from 1961 to 1962 and then as president from 1964 to 1985, He was born in April 1922 and passed away in october 1999. Then he led Tanzania as the president from 1964 to 1985